# MAHALI PALIPO ANDALIWA KWA AJILI YAKO

## UTANGULIZI

Kulikuwa na mtu aliyeitwa Yesu Kristo, ambaye alikuwa Mungu aliyedhihirishwa katika mwili (1 Timotheo 3:16). Maisha yake yalibadilisha ulimwengu kiasi kwamba mfumo wa kalenda wa kuweka tarehe ulibadilishwa kuwa B.C (Kabla ya Kristo), na A.D (Kigiriki *Anno Domini*, "katika mwaka wa Bwana wetu" ) kuonyesha kiwango cha jinsi maisha yake yalibadilisha ulimwengu tunaoishi ndani.

Hakufanya tu miujiza alipoishi duniani, lakini alijiruhusu mwenyewe kuuawa kwa ajili yetu. Alipenda watu aliokuwa amewafanya kiasi hicho. Habari za kuchangamsha ni kwamba alifufuka kutoka kwa wafu. Neno lake hutwambia katika:

**Matendo 1:3**
Wale aliwadhihirishia nafsi yake, kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa kwake, ya kwamba yu hai, akiwatokea muda wa siku arobaini, na kuyanena mambo yaliyouhusu ufalme wa Mungu.

**Yesu Kristo alifanya ahadi maalum kwa wote walio mfuata katika maisha haya. Alisema:**

**Yohana 14:2-3**
Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo.

**Mathayo 24:35**

**Yesu Kristo alisema zaidi...**

Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe.

Mpango wa wokovu, jinsi mtu anaweza ridhi mahali ambapo Yesu anasema ameenda kutuandalia, hautabadilika, tangu wakati yeye na wanafunzi waliunena, hadi mwisho wa wakati.

**Zaburi 119:89**
Ee Bwana, neno lako lasimama imara mbinguni hata milele.

## MAFUNZO HAYA YANAONYESHA JINSI UNAWEZA KURITHI MAHALI PALE PALIPOANDALIWA...

### KUZALIWA MARA YA PILI

Kwa watu wengi ni vigumu kuwa na ufahamu wa kiroho kwamba Yesu Kristo ameandaa mahali kwa wale wote wanaomfuata. Ufahamu wa mwanadamu pekee haujatosha kuwa na kuelewa kwa kiroho kwa Biblia.

Biblia inasema:

**1 Wakorintho 2:14**
Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni.

Kama tu vile mtoto ambaye hajazaliwa hawezi kufahamu wazazi wakimfundisha jinsi ya kukubali upendo wao, utunzaji, chakula na nyumba hadi baada ya kuzaliwa, vivyo hivyo ni kweli na ufahamu wetu wa Mungu na Biblia. Ili sisi kwa hakika tufahamu, mtu lazima azaliwe tena kiroho! Wacha tusome kile Yesu alisema kwa mtu aliyeitwa Nikodemo...

**Yohana 3:3-7, 9, 12**
Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin nakuambia, mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu. Nikodemo akamwambia, Awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa? Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu. Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho. Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, Hamna budi kuzaliwa mara ya pili. Nikodemo akajibu, akamwambia, Yawezaje kuwa mambo haya? Yesu akajibu, akamwambia, ikiwa nimewaambia mambo ya duniani, wala hamsadiki, mtasadiki wapi niwaambiapo mambo ya mbinguni?

Katika maandiko haya, Yesu anatufundisha kwamba ili kuingia mbinguni ni LAZIMA tuzaliwe mara ya pili kwa maji na Roho. Kwa kuwa tunajua haiwezekani kwa Mungu kusema uongo (**Waebrania 6:1-8),** tunaweza jua kila mmoja wetu lazima azaliwe tena kama alivyomfundisha Nikodemo...

Inawezekanaje kuzaliwa mara ya pili? Injili ya Yesu Kristo inatuonyesha.

**Luka 18:27**
Yesu akasema, yasiyowezekana kwa wanadamu yawezekana kwa Mungu.

**Yohana 5:39**
Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia.

Kwa maneno mengine, tunataka kuhakikisha kwamba tunafuata mpango ambao Yesu anatufundisha kupitia Biblia ili tuwe tumejiandaa kwa mahali alipo napo kwa ajili yetu. Anatuacha tujue umuhimu wa kutubu na kuamininenо la Mungu.

## TOBA NI UAMUZI

**Warumi 3:23**
Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;

**Warumi 6:23**
Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.

**Warumi 5:12**
Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi:

**Marko 1:15**
Akisema, Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili. (Amini katika kiyunani cha mwanzo humaanisha mtu binafsi kujitoa kabisa kwa).

“Akili iliyo amua.” Tunabadilisha nia yetu na akili yetu na matendo yetu kuhusu dhambi (mabadiliko ya ndani yatajionyesha nje kwa wengine na kwetu sisi wenyewe kwamba tumeamua kumfuata Yesu na kutii neno lake).

Hatua ya kwanza ya kuzaliwa mara ya pili ni kutubu na kuamini injili. Hatua inayofuata ni kuzaliwa mara ya pili kwa maji.

## JINSI YA KUZALIWA KWA MAJI

Kuna mifano mikubwa katika Biblia ya watu wakizaliwa mara ya pili kwa maji.

**Matendo 8:30-31**
Basi Filipo akaenda mbio, akamsikia anasoma chuo cha nabii Isaya; akanena, Je! Yamekuelea haya unayosoma? Akasema, Nitawezaje kuelewa, mtu asiponiongoza? Akamsihi Filipo apande na kuketi pamoja naye.

**Matendo 8:35-39**
Filipo akafunua kinywa chake, naye, akianza kwa andiko hilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu. Wakawa wakiendelea njiani, wakafika mahali penye maji; yule towashi akasema, Tazama, maji haya; ni nini kinachonizuia nisibatizwe? Filipo akasema, Ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana. Akajibu, akanena, Naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu. Akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi; naye akambatiza. Kisha, walipopanda kutoka majini, Roho wa Bwana akamnyakua Filipo, yule towashi asimwone tena; basi alikwenda zake akifurahi.

Katika maandiko haya, tunaona mtu akizaliwa kwa maji (kubatizwa). Agano Jipya mwanzo iliandikwa katika lugha ya Kiyunani kisha ikatafsiriwa katika kiingezrza na lugha zingine. Neno la kiyunani kwa kubatizwa ni baptizo: kuzamisha, tosa, kugharikisha (yaani kuloweka kabisa). Yesu alitwambia katika:

**Marko 16:16**
Aaminiye na kubatizwa ataokoka.

Hapa kuna baadhi ya mifano zaidi ya watu wakibatizwa (kuzaliwa kwa maji) na kile kilisemwa walipokuwa wakibatizwa.

**Matendo 2:37-41**
Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu? Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie. Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya, akisema, Jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi. Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu.

Mtume Petro alijua umuhimu wa sio tu toba, lakini pia kubatizwa katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi. Mifano ingine inapatikana katika:

**Matendo 8:12**
Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa, wanaume na wanawake.

**Matendo 10:47, 48**
Ni nani awezaye kuzuia maji, hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi? Akaamuru wabatizwe kwa Jina lake Yesu Kristo. Ndipo wakamsihi azidi kukaa siku kadha wa kadha.

Hapa tena tunaona maji na ubatizo ukifanywa katika jina la Bwana [Yesu]. Kubatizwa katika jina la Yesu ni kimaandiko. Ni ujuzi wa kuchangamsha kuliko chochote kingine. Kuwa na ondoleo la dhambi ni bure bila malipo.
**Matendo 19:5**

Waliposikia haya wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu.

**Matendo 22:16**
Basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe , ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake.

**Warumi 6:3-4**
Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.

Kwa hivyo, hatua ya pili ya kuzaliwa mara ya pili ni kubatizwa kwa kutumbukizwa katika jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi.

**Hatua inayofuata ni kuzaliwa mara ya pili kwa Roho.**

## JINSI YA KUZALIWA KWA ROHO

Tangu nyakati za Agano la Kale, tunaweza soma kwamba ilikuwa mpango wa Mungu kila wakati kwa watu wake kubadilishwa na ujuzi ambao Masihi angeleta.

**Isaya 28:11-12**
La, bali kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine atasema na watu hawa; ambao aliwaambia, Hii ndiyo raha yenu, mpeni raha yeye aliyechoka; huku ndiko kuburudika; lakini hawakutaka kusikia.

**Yoeli 2:28**
Hata itakuwa, baada ya hayo, ya kwamba nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili; na wana wenu, waume kwa wake watatabiri...

Vile vile, Yesu Kristo alifundisha...

**Matendo 1:5**
Ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache.

**Marko 16:17**
Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;

Yesu aliwaambia wanafunzi kwamba moja wapo wa ishara zitakazo mfuata muumini wa kweli ni kwamba huyo mtu atanena na lugha mpya. (Neno la mwanzo la kiyunani lililotumiwa kwa ndimi ni glossa, lugha).

**Yohana 3:8**
Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho.

**TAMBUA**: Upepo, Roho na Roho(Ghost) katika Kiyunani ni *pneuma*; Neno hili pia linatafsiriwa kama Roho wa Kristo, Roho Mtakatifu, Upepo na Roho.

**TAMBUA**: Sauti katika Kiyunani ni *Phone*; Maana ya hili neno katika Kiyunani inaweza kuwa sauti [sauti ya maneno yaliyonenwa] namna ya tabia ya sauti, sauti, usemi [lugha au ulimi].

Yohana 3:8 inatwambia kwamba wakati mtu anapojazwa na Roho, kutakuwa na sauti ambayo ni Upepo (Roho) pekee unaweza fanya. II Wakorintho 5:17 pia inasema tutakuwa mtu tofauti na mpya.

**Yohana 10:10**
Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.

Zaidi ya kuwa na mahali palipoandaliwa kwa wale wanaofuata mpango huu, alikuja ili tuwe na maisha bora zaidi na yenye manufaa zaidi katika ulimwengu huu wa kweli.

**Matendo 1:8**
Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katikaYerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.

Hii nguvu itaturuhusu kunena kwa uhuru na kwa nguvu kuhusu kile kimefanyika kwetu na jinsi Roho wa Mungu ametubadilisha. Nguvu hii pia itatupatia kile tunakosa ili kushinda dhambi ikiwa tutaiweka ikiwa mpya na yenye kufanya kazi katika maisha yetu.

**Matendo 2:1-4**
Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka.

Huu ndio ujuzi wa kuzaliwa kwa Roho ambao Yesu aliuzungumzia katika Yohana 3:5.

**Matendo 8:14-17**
Na mitume waliokuwako Yerusalemu, waliposikia ya kwamba Samaria imelikubali neno la Mungu, wakawapelekea Petro an Yohana; ambao waliposhuka, wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu; kwa maana bado hajawashukia hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa jina lake Bwana Yesu. Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu.

Kilicho fanyika kwa waumini ni cha kupendeza. Walibatizwa, kwa hivyo tunafahamu kwamba kabla ya ubatizo wao walikuwa wametubu. Walikuwa wameamini injili na kutii lakini kulikuwa na kitu kimoja hawakuwa nacho bado. Hawakupokea Roho Mtakatifu walipotubu, hawakuipokea walipo batizwa, waliipokea tu baada ya wanafunzi kuja kutokaYerusalemu, wakawawekea mikono na kuwaombea waipokee. Hili silo lililofanyika katika kila mfano tunaouona katika Agano Jipya wa watu wakipokea Roho Mtakatifu lakini linatuonyesha kwamba ile kuzaliwa kwa Roho (Yohana 3:5) ni ujuzi ulio kando sana na tofauti na toba na ubatizo. Wakati Wasamaria walizaliwa kwa Roho haijatajwa kuhusu kunena katika lugha nyingine. Hata ingawa hakukutajwa, Filipo alijuaje hawakuwa wamepokea Roho Mtakatifu na ni jinsi gani wanafunzi walijua wakati waliipokea? Walikuwa wakitafuta ile ishara iliyokuja wakati wao wenyewe walipokea Roho Mtakatifu.

**Matendo 10:44-48**

Petro alipokuwa akisema maneno hayo, Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia lile neno. Na wale waliotahiriwa, walioamini, wakashangaa, watu wote waliokuja pamoja na Petro, kwa sababu Mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha, na kumwadhimisha Mungu. Ndipo Petro akajibu, ni nani awezaye kuzuia maji, hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi? Akaamuru wabatizwe kwa Jina lake Yesu Kristo. Ndipo wakamsihi azidi kukaa siku kadha wa kadha.

Kwa kuwa roho haiwezi kuonekana, kama upepo, Petro na marafiki zake hawangejua ikiwa watu hawa walikuwa wamepokea Roho Mtakatifu. Lakini, kulikuwa na ishara, sauti iliyokuja wakipokea Roho Mtakatifu. Ishara hiyo ilikuwa walinena katika lugha ambayo hawakuijua.

Katika nyumba ya Kornelio, Roho Mtakatifu alipokewa kabla hawajabatizwa. Tambua kwamba kitu cha kwanza Petro anasema baada ya kuona na kuwasikia wakizaliwa kwa Roho, ni kwamba wote walihitaji kubatizwa katika maji, katika jina la Yesu.

**Matendo 19:2, 3, 5-7**

Akawauliza, Je! Mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini? Wakamjibu, La, hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia. Akawauliza, Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani? Wakasema, Kwa ubatizo wa Yohana. Waliposikia haya wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu. Na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao; wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri. Na jumla yao walipata wanaume kumi na wawili.

Wakati Paulo alipata waumini hawa maswali mawili ya kwanza aliyowauliza yalikuwa, kwa Paulo, yaliyo ya muhimu zaidi. Mlibatizwa kwa ubatizo gani, na je mmepokea Roho Mtakatifu?

**Mathayo 7:21-23**

Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu.

Kumalizia, usiwe mtu anaye omba, enda kanisani, ona miujiza, na hata mahubiri, lakini hauingii **mahali Yesu amekuandalia** kwa sababu haukuzaliwa mara ya pili kama vile maandiko yanafundisha. MWISHO.